Somo la 26　次はがんばろう
TSUGI　WA　GANBARÔ

アンナ	ロドリゴ、元気がないね。	Rodrigo, unaonekana hauko sawa.
Anna	RODORIGO,　GENKI　GA　NAI　NE.	
ロドリゴ	試験ができなかったんです。	Sikufanya vizuri katika jaribio.
Rodrigo	SHIKEN　GA　DEKINAKATTA　N DESU.	
アンナ	私も・・・。６０点でした。	Mimi pia….
Anna	次はがんばろう。	Nimepata alama 60.
	WATASHI　MO….	Tujitahidi wakati mwingine.
	ROKUJITTEN　DESHITA.	
	TSUGI　WA　GANBARÔ.	

Vidokezo vya sarufi

①　_ N DESU

◈ Unasema N DESU, unapoelezea hali au sababu.

◈ Kabla ya N DESU, unatakiwa kutumia muundo wa kawaida wa kitenzi, kama vile umbo la kikamusi na umbo la TA.

k.m.) SHIKEN GA DEKINAKATTA N DESU.（Sikufanya vizuri katika jaribio.）

↳ Muundo wa kawaida wa DEKIMASEN DESHITA (kutofanya vizuri)

②　DESHITA : Umbo la wakati uliopita la DESU

k.m.)　TAIHEN DESU. (Ni vigumu.) ⇒ TAIHEN DESHITA. (Ilikuwa vigumu.)

③　GANBARÔ　(Tujitahidi)　☞ *Vitenzi : uk.54, 55*

◈ GANBARÔ ni umbo la kuonyesha nia la kitenzi cha GANBARIMASU (kujitahidi).

◈ Umbo la kuonyesha nia linaelezea dhamira ya mzungumzaji. Pia hutumika kumshirikisha msikilizaji kufanya jambo fulani pamoja, au kumtaka afanye jambo fulani.

Tanakali Sauti

Mtoto mchanga analia sana.

Mtoto analia kwa sauti.